



**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



*Sokwe kwenye Hifadhi ya Taifa ya Gombe. Uhifadhi wa baionuai husaidia wanyamapori na jamii zinazowazunguka.  
Picha na: USAID/Jessica Padron*

## TANZANIA

# UTUNZAJI WA ARDHI TANZANIA MAGHARIBI

Kwa kushirikiana na Taasisi ya Jane Goodall (JGI), mradi wa utunzaji wa ardhi magharibi mwa Tanzania, unafanya kazi ya kulinda Sokwe walio hatarini, pamoja na kulinda makazi yao kwa kutumia namna mbalimbali, kama mipango ya matumizi bora ya ardhi, kuwawezesha wananchi kuwa na maisha bora katika vijiji vinavyozunguka Gombe, Masito na Ugalla. Maeno ya Gombe –Masito –Ugalla yanakadiriwa kuwa na sokwe zaidi ya asilimia tisini ya idadi yote ya sokwe takribani 2,200 walioko ukanda wa magharibi mwa Tanzania.

Jamii hii muhimu ya sokwe inakabiliwa na vitisho vinayoongezeka katika makazi yao vinavyotokana na uvunaji hovyoo wa miti, kupanuka kwa makazi ya watu, kugeuzwa misitu asili kuwa maeneo ya kilimo na kadhhalika. Sokwe wako hatarini pia kupata maambukizi ya magonjwa kutoka kwa binadamu pamoja na migogoro kati ya wanyama na binadamu.

Ongezeko la vitisho hivi huchangiwa na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaosababisha uvunaji wa maliasili usio na mpangilio maalumu, hii inatokana na serikali kutokua na uwezo wa kutosha kusimamia maliasili ipasavyo ambayo hupelekea matokeo hafifu ya uhifadhi.

Ukiongozwa na mpangokazi thabiti wa JGI wa kutunza Sokwe, katika ngazi ya mkoa na kitaifa, shughuli za mradi wa LCWT zitaongezeka kutoka vijiji 74 vya awali hadi kufikia vijiji 104 katika wilaya za Kigoma na Uvinza mkoani Kigoma, na wilaya za Tanganyika na Mpanda mkoa wa Katavi. Hii inajumuisha yaliyokuwa makazi ya wakimbizi ya Katumba na Mishamo.

Shughuli za mradi zinajumuisha:

- **Usimamizi wa Maliasili:** Kujengea uwezo serikali za wilaya na vijiji ili kuwezesha uhifadhi kwa vitendo na ufanisi katika kusimamia maliasili.
- **Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Maendeleo Endelevu:** Kusaidia serikali za wilaya na vijiji, na jamii kutekeleza mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi na katika kujikimu kimaisha.
- **Watu, Afya na Mazingira:** Kuendeleza shughuli ili kuboresha ufahamu na upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango na afya ya uzazi.
- **Ufuatiliaji:** Kuboresha ufuatiliaji wa malengo ya uhifadhi, maendeleo na vitisho kwa kutumia teknolojia za ubunifu katika kukusanya, kuchambua na kuchakata taarifa na takwimu, na kutoa tahadhari kama sehemu ya mfumo wa msaada wa maamuzi. Taarifa kutoka kwenye huu mfumo utawezesha JGI na wadau wa ndani kuchunguza, kuthibitisha na kutatua pamoja na kufanya maamuzi ambayo yatasaidia shughuli za LCWT.
- **Elimu ya Mazingira:** kutanua uenezi na ufanisi wa kuhamasisha jamii juu ya elimu ya mazingira ili kuhamasisha mabadiliko ambayo yatalinda sokwe na makazi yao.

**BAJETI** Dola za Kimarekani milioni 19.9

#### **MUDA**

Novemba 2018 – Novemba 2023

#### **MAENEO YA MRADI**

Mikoa ya Kigoma na Katavi

#### **MBIA MTEKELEZAJI**

Taasisi ya Jane Goodall

#### **WABIA**

Pathfinder International

RTI International

#### **MAWASILIANO YA USAID**

Jestina Kimbesa

Mtaalamu wa usimamizi wa Mradi

[jkimbese@usaid.gov](mailto:jkimbese@usaid.gov)

Munzero Kanyangemu

Mtaalamu wa Baionuai

[mkanyangemu@usaid.gov](mailto:mkanyangemu@usaid.gov)

#### **MAWASILIANO YA JGI**

Emmanuel Mtiti

Mkurugenzi Mkuu Mipango na Sera

[emtiti@janegoodall.or.tz](mailto:emtiti@janegoodall.or.tz)

Tovuti: [www.janegoodall.org](http://www.janegoodall.org)

Facebook: @janegoodallinst

Twitter: @JaneGoodallInst

#### **KWA TAARIFA ZAIDI**

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAID Tanzania

Twitter: @USAIDTanzania